TANGAZO LA SERIKALI Na. 862 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 80)*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA MJI WA KIHISTORIA WA MIKINDANI NA MAENEO MENGINE YA URITHI YALIYOHIFADHIWA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 218 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Mji wa Kihistoria wa Mikindani na Maeneo Mengine ya Urithi Yaliyohifadhiwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Mji wa Kihistoria wa Mikindani na Maeneo Mengine ya Urithi Yaliyohifadhiwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu"

Kuongeza kifungu wezeshi

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kuongeza kabla ya kichwa cha habari cha Sheria Ndogo kuu kifungu wezeshi kifuatacho:

*"(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 80)".*

Marekebisho ya kanuni ya 3

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri mpya ifuatayo kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti:

Sura ya 281

""Bodi" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Makumbusho ya Taifa;".

Marekebisho ya kanuni ya 21

**4**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 21 kwa kufuta neno "unaofaa" na badala yake kuweka maneno "wa siku ishirini na moja".

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*